

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P. 1175

DODOMA

Simu: 026 2322846

Nukushi: 026 2320003

Baruapepe: rbcdodoma@pccb.go.tz

www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

WALIOHUJUMU MRADI WA UKARABATI WA MIUONDOMBINU YA MAJI NTOMOKO KONDOA WAFIKISHWA MAHAKAMANI

TAKUKURU Mkoa wa Dodoma tarehe 10/10/2018 imewafikisha Mahakamani **Bw. Abas Musa Mahuna - Mkurugenzi wa Kampuni ya Ushauri ya POA na Ali Hussein Mruma aliyekuwa Mhandisi wa Maji - Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa** na kufunguliwa kesi ya Uhujumu Uchumi Na. 44/2018.

Akiwasomea mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama Wilaya ya Dodoma **Mhe Mery Sanapee**, Mwendesha Mashtaka Mwandamizi wa Serikali Bw. **Josephat Mkizungo** aliiambia Mahakama kuwa washtakiwa wametenda makosa ya kutumia nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri kinyume na Kifungu cha 22; Kushirikiana na kutenda kosa kinyume na Kifungu cha 30; Matumizi mabaya ya madaraka kinyume na kifungu cha 31; Kula njama kinyume na kifungu cha 32; vyote vikiwa ni vifungu chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007; Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 1984 pamoja na Sheria ya Makosa ya Utakatishaji wa Fedha Na. 12 ya Mwaka 2006.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, mtuhumiwa Abasi Musa Mahuna - Mkurugenzi POA Engineers Pte Company na Ali Hussein Mruma aliyekuwa Mhandisi wa Maji Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, waliandaa hati za malipo zilizokuwa na taarifa za uwongo na kupitisha malipo kwa ajili ya mradi wa maji Ntomoko yenye thamani ya **Tshs. 1,657,953,557/=**

Aidha Mwendesha Mashitaka alisema kuwa Washtakiwa wote wawili wametenda kosa la Kutakatisha Fedha kinyume na Sheria na 12 ya Mwaka 2006.

Washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu lolote kwani Mahakama ya Hakimu Mkazi - Wilaya ya Dodoma haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi. Washtakiwa walipelekwa Gerezani hadi tarehe 22/10/2018 kesi yao itakapokuja kwa ajili ya kutajwa. Washtakiwa wa kesi hii ni miongoni mwa washtakiwa wengine watano (05) waliofikishwa Mahakamani mnamo tarehe 8/10/2018 kwa makosa ya Kutakatisha Fedha na ufujaji wa fedha kwenye Mradi wa Maji Ntomoko Wilaya ya Kondoa.

Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Dodoma **Bw Musa Chaulo** amewashukuru wananchi wa mkoa wa DODOMA kwa kushirikiana na TAKUKURU na amewataka wananchi na watumishi wote wanaopewa dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mkoa wa Dodoma kutofanya ubadhirifu, na kwamba yeyote atakayethubutu kutenda kosa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake..

Imetolewa na:

Bw. Musa Chaulo –Naibu Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma